TANGAZO LA SERIKALI Na. 1074 la tarehe 20/12/2024

SHERIA YA PETROLI
(SURA YA 392)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128(3))*

NOTISI YA KIBALI CHA UJENZI WA KITUO KIKUU CHA GESI ASILIA ILIYOSHINDILIWA KWA KAMPUNI YA ENERGO PEMBENI YA BARABARA YA MWENGE – COCA COLA MANISPAA YA KINONDONI YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kibali cha Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Gesi Asilia Iliyoshindiliwa kwa Kampuni ya Energo Pembeni ya Barabara ya Mwenge – Coca Cola Manispaa ya Kinondoni ya mwaka 2024.

Tafsiri

**2**. Katika Notisi hii isipokuwa kama mukhtadha unahitaji vinginevyo-

"mwombaji" maana yake ni kampuni ya Energo wa S.L.P. 653 Dar es Salaam;

Sura ya 392

"kibali" maana yake ni kibali cha ujenzi kilichotolewa na Mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 128(1) cha Sheria ya Petroli; na

Sura ya 414

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji.

Kutolewa kwa kibali

**3**. Kibali kimetolewa kwa mwombaji kujenga kituo kikuu cha gesi asilia iliyoshindiliwa pembeni ya Barabara ya Mwenge – Coca Cola Manispaa ya Kinondoni kwa vigezo na masharti yafuatayo:

(a) kuzingatia michoro iliyopitishwa, viwango vya kiufundi, ujenzi, uchomeleaji, upimaji na uidhinishaji, na njia iliyowekwa alama au sheria zingine zinazotumika;

(b) kuhakikisha kituo au miundombinu mingine inayohusika inajengwa kwa kuzingatia viwango vyote vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Taifa au sheria zingine zinazohusika;

(c) kuhakikisha ukaguzi wa mahitaji ya ujenzi wa vituo vya kujaza gesi au miundombinu mingine inayohusika inakidhi uzingatiaji wa vifaa, ujenzi, uchomeleaji, uunganisho na majaribio kulingana na viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango la Taifa;

(d) kuhakikisha hakuna au kupunguza usumbufu kwa wakazi walio karibu na eneo la kituo na usalama kwa umma upewe kipaumbele.

(e) iwapo ulipuzi utafanyika, ufanyike kwa kuzingatia taratibu za kisheria zilizopo na kufanywa na mtu mwenye sifa za kazi ya ulipuzi na kwa kuzingatia usalama kwa umma, mifugo, wanyama, majengo, miundombinu ya simu, umeme, miundombinu ya chini ya ardhi na mali nyingine yoyote iliyo karibu na eneo la ulipuzi;

(f) kuhakikisha kufanyika kwa juhudi za kupunguza uharibifu kwenye eneo la ujenzi na kuzuia mazingira yatakayosababisha kuziba kwa mifereji ya kupitisha maji na mmomonyoko wa udongo na baada ya ujenzi, ardhi itapaswa kurudishwa katika hali iliyokuwepo kwa kadri itakavyowezekana;

(g) kuzingatia viwango vya mazingira, afya na usalama vilivyoainishwa na sheria zinazohusika;

(h) uzingatiaji wa afya na usalama wa watu na vifaa na kuhakikisha matumizi ya vifaa vya usalama kama vile kofia ngumu, miwani na viatu vya usalama na matumizi ya kizima moto kwa wakati wote; na

(i) kuhakikisha kuwa miundombinu yote bila kujali kuwa inadhibitiwa na Mamlaka au la

inalindwa dhidi ya uharibifu na kuwaomba waendeshaji wa miundombinu hiyo wawepo eneo la ujenzi wakati wa ujenzi.

Ukomo

**4**. Kibali kilichotolewa katika Notisi hii kitakoma endapo mwombaji hataanza ujenzi ndani ya miezi ishirini na nne tangu tarehe ya kutolewa kwake.

Dodoma, ......................, 2024

JAMES A. MWAINYEKULE,
*Mkurugenzi Mkuu*